# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# MUHTASARI WA SOMO LA STADI ZA KAZI
# ELIMU YA MSINGI DARASA LA V-VII

**2019**

© Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, 2015

Toleo la kwanza, 2015
Toleo la pili, 2016
Toleo la tatu, 2019

ISBN 978-9987-09-060-0

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P 35094
Dar es Salaam

Simu: +255 22 2773005/+255 22 277 1358
Faksi: +255 22 2774420
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejelewe kama: Taasisi ya Elimu Tanzania. (2015). Muhtasari wa Somo la Stadi za Kazi Elimu ya Msingi Darasa la V-VII. Dar es Salaam: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha wala kufasiri andiko hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi ya Kamishna wa Elimu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

# Yaliyomo


Dibaji ........ iv
Orodha ya majedwali ........ v
1. Utangulizi ........ 1
2. Uhusiano kati ya muhtasari huu na Mtaala wa Elimu ya Msingi ........ 1
2.1 Malengo ya Elimu ya Msingi ........ 1
2.2 Umahiri wa Elimu ya Msingi Darasa la III-VII ........ 2
2.3 Malengo ya Somo la Stadi za Kazi ........ 2
2.4 Umahiri mkuu na umahiri mahususi katika Somo la Stadi za Kazi ........ 3
2.5 Ufundishaji na ujifunzaji wa Somo la Stadi za Kazi ........ 4
2.6 Upimaji wa ujifunzaji ........ 4
3. Maudhui ya muhtasari ........ 4
3.1 Umahiri mkuu ........ 4
3.2 Umahiri mahususi ........ 4
3.3 Shughuli za mwanafunzi ........ 5
3.4 Vigezo vya upimaji ........ 5
3.5 Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi ........ 5
3.6 Idadi ya vipindi ........ 5
4. Maudhui ya Darasa la V ........ 6
5. Maudhui ya Darasa la VI ........ 25
6. Maudhui ya Darasa la VII ........ 42

## Dibaji

Elimu bora ni haki ya kila Mtanzania. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imekuwa ikiboresha Mtaala wa Elimu ya Msingi kuhakikisha kwamba elimu inayotolewa ni bora na inayomwandaa mwanafunzi kumudu maisha katika mazingira yake. Muktadha huu umewezesha Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuboresha mchakato wa kufundisha na kujifunza Somo la Stadi za Kazi kwa kuandaa muhtasari huu. Muhtasari wa Somo la Stadi za Kazi umeandaliwa kwa kuzingatia Mtaala wa Elimu ya Msingi Darasa la I -VII wa mwaka 2015 toleo la mwaka 2019. Muhtasari huu unasisitiza kufundisha na kujifunza kunakozingatia ujenzi wa umahiri kwa mwanafunzi. Kwa kutumia muhtasari huu, mwanafunzi atajenga stadi za uchunguzi, udadisi, utumiaji wa taarifa za uchunguzi, kukuza stadi za ubunifu na ugunduzi wa kisayansi na kiteknolojia.

Muhtasari wa Somo la Stadi za Kazi una vipengele mbalimbali vinavyojumuisha umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za kutendwa na mwanafunzi, vigezo na viwango vya upimaji pamoja na idadi ya vipindi kwa kila umahiri mahususi. Vipengele hivi vitamsaidia mwalimu kutambua namna ya kufundisha na kupima utendaji wa mwanafunzi kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri. Hata hivyo, umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) unaendelea kupewa msisitizo katika Somo la Stadi za Kazi.

Mwalimu anatarajiwa kutumia muhtasari huu kwa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa. Hata hivyo, anaweza kupanga utekelezaji wa muhtasari kwa kuzingatia mazingira yanayomzunguka.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inaendelea kupokea maoni ya kuboresha muhtasari huu kutoka kwa walimu na wadau wengine wa elimu. Maoni yote yapelekwe kwa Mkurugenzi Mkuu Taasisi ya Elimu Tanzania.

…………………………...………

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
**Kaimu Kamishna wa Elimu**
**Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

# Orodha ya majedwali


Jedwali Na. 1 Umahiri utakaojengwa kwa mwanafunzi katika Somo la Stadi za Kazi .......................................... 3

Jedwali Na. 2 Umahiri utakaojengwa na mwanafunzi katika Darasa la V ............................................................ 6

Jedwali Na. 3 Maudhui ya muhtasari Darasa la V ........................................................................................ 7

Jedwali Na. 4 Umahiri utakaojengwa na mwanafunzi katika Darasa la VI .......................................................... 25

Jedwali Na. 5 Maudhui ya muhtasari Darasa la VI ...................................................................................... 26

Jedwali Na. 6 Umahiri utakaojengwa na mwanafunzi katika Darasa la VII ......................................................... 42

Jedwali Na. 7 Maudhui ya muhtasari Darasa la VII ..................................................................................... 43

## 1.0 Utangulizi

Muhtasari wa Somo la Stadi za Kazi umeandaliwa kwa kuzingatia Mtaala wa Elimu ya Msingi wa mwaka 2015, toleo la tatu la mwaka 2019. Muundo wa sasa wa Somo la Stadi za Kazi ulianza mwaka 2016. Katika mwaka huo, Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia ilibadilisha namna ya kufundisha somo hili. Mabadiliko yaliyojitokeza katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo hili ni pamoja na kufundisha stadi mbalimbali kwa ujumla wake badala ya ufundishaji wa kimasomo kama ilivyokuwa hapo awali. Tafiti zinaonesha kuwa kabla ya mwaka 2016, ufundishaji wa kimasomo ulisababisha wanafunzi kupata maudhui kwa vipande vipande hivyo kushindwa kujenga umahiri uliotarajiwa.

Somo la Stadi za Kazi linalenga kumjengea mwanafunzi maarifa, stadi na mwelekeo utakaomwezesha kukabiliana na mazingira yanayomzunguka katika maisha ya kila siku. Ufundishaji wa somo hili umelenga kumwezesha mwanafunzi kujenga umahiri hatua kwa hatua kulingana na darasa husika. Somo hili linalenga kubaini vipaji vya mwanafunzi na kuviendeleza, kujenga misingi ya kujitegemea, kuhimiza ubunifu na kutambua fursa zilizopo katika mazingira na kuzitumia. Muhtasari huu umegawanywa katika sehemu kuu tatu ambazo ni utangulizi, maelezo ya jumla ya mtaala na maudhui ya muhutasari.

## 2.0 Uhusiano kati ya Muhtasari huu na Mtaala wa Elimu ya Msingi

Mtaala wa Elimu ya Msingi umebainisha mambo mbalimbali ikiwemo umahiri mkuu na umahiri mahususi katika kila somo kwa Darasa la III-VII. Muhtasari wa Stadi za Kazi umewasilisha baadhi ya vipengele vya mtaala ambavyo ni malengo ya Elimu ya Msingi, umahiri wa Elimu ya Msingi, malengo ya Somo la Stadi za Kazi, umahiri mkuu na mahususi, ufundishaji na ujifunzaji wa Somo la Stadi za Kazi na upimaji wa ujifunzaji. Pamoja na vipengele hivi, muhtasari huu umechakata na kubainisha kwa kina maudhui, shughuli za mwanafunzi, vigezo vya upimaji, viwango vya utendaji, na idadi ya vipindi. Ufafanuzi huu utamwezesha mwalimu kuelewa na kutumia muhtasari huu kufundisha kwa ufasaha Somo la Stadi za Kazi.

### 2.1 Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la III-VII

Elimu ya Msingi ina madhumuni ya kuwapatia walengwa maarifa, stadi na mielekeo inayohitajika kwa maendeleo ya Watanzania. Malengo makuu ya Elimu ya Msingi ni kumwezesha mwanafunzi:

a) kukuza stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu na kuwasiliana;
b) kuifahamu, kuitumia na kuithamini lugha ya Kiswahili;

c) kufahamu misingi ya utawala wa sheria;
d) kuthamini utamaduni wa Kitanzania na wa jamii nyingine;
e) kukuza uwezo wa mwanafunzi kufikiri, kubuni, na kutatua matatizo;
f) kutambua umuhimu wa maadili, uadilifu na uwajibikaji kama misingi ya raia mwema;
g) kushiriki katika shughuli za michezo na sanaa pamoja na kuthamini kazi za kisanii;
h) kubaini na kukuza vipaji na vipawa vyake;
i) kuthamini na kupenda kufanya kazi;
j) kutambua, kuthamini na kutumia sayansi na teknolojia; na
k) kujiandaa kwa ngazi nyingine ya elimu pamoja na kujifunza kusiko na kikomo.

## 2.2 Umahiri wa Elimu ya Msingi Darasa la III-VII

Umahiri wa Elimu ya msingi umejikita katika kumwandaa mwanafunzi kuwa na uwezo wa:

a) kuwasiliana kwa ufasaha kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwa kuzungumza na kuandika;
b) kusoma kwa kujiamini na kufahamu maandishi sahili;
c) kutumia dhana na kanuni za kihisabati katika maisha ya kila siku;
d) kutumia stadi za kisayansi, kiteknolojia na kiufundi katika maisha halisi ya kila siku;
e) kutumia utamaduni wake na wa jamii nyingine;
f) kuheshimu tofauti za kiimani na kiitikadi katika jamii;
g) kushiriki katika michezo na shughuli za kisanii;
h) kujiheshimu na kuheshimu wengine;
i) kutumia mising ya kizalendo katika maisha ya kila siku;
j) kushiriki katika kazi mbalimbali zinazoendana na umri wake;
k) kushiriki katika shughuli zinazokuza uwezo wake wa kufikiri kimantiki na kiyakinifu; na
l) kushirikiana na wengine kwa kufanya matendo yanayokubalika katika jamii.

## 2.3 Malengo ya Somo la Stadi za Kazi

Malengo makuu ya ufundishaji wa Somo la Stadi za Kazi kwa mwanafunzi wa Darasa la V-VII ni:

a) kubaini vipaji vya wanafunzi na kuviendeleza;

b) kujenga misingi ya kujitegemea;
c) kuwa mbunifu; na
d) kutambua fursa katika mazingira yake.

### 2.4 Umahiri mkuu na umahiri mahususi katika Somo la Stadi za Kazi

Sehemu hii inawasilisha umahiri katika somo kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 1:

**Jedwali Na. 1: Umahiri utakaojengwa kwa mwanafunzi katika Somo la Stadi za Kazi**

| **Umahiri Mkuu** | **Umahiri Mahususi** |
|---|---|
| 1.0 Kuwa nadhifu | 1.1 Kujenga tabia ya usafi wa mwili<br>1.2 Kutunza mavazi katika kudumisha usafi<br>1.3 Kutunza mazingira katika kudumisha makazi safi |
| 2.0 Kumudu mapishi mbalimbali | 2.1 Kutambua kanuni zinazohitajika katika mapishi<br>2.2 Kutayarisha vyakula aina tofauti<br>2.3 Kutengeneza vinywaji tofauti |
| 3.0 Kusanifu kazi za sanaa | 3.1 Kumudu misingi ya uimbaji na uigizaji<br>3.2 Kutengeneza picha zenye ujumbe tofauti kwa jamii<br>3.3 Kubuni chapa mbalimbali za sanaa za ufundi<br>3.4 Kufinyanga maumbo mbalimbali<br>3.5 Kutengeneza vitu kwa kutumia makuzi mbalimbali |
| 4.0 Kufahamu stadi za ujasiriamali | 4.1 Kujenga utayari wa kujifunza<br>4.2 Kutafuta masoko ya bidhaa ndogondogo<br>4.3 Kutambua kanuni za usimamizi wa fedha |

## 2.5 Ufundishaji na ujifunzaji wa Somo la Stadi za Kazi

Kufundisha na kujifunza Somo la Stadi za Kazi kutaongozwa na ujenzi wa umahiri kwa kutumia mbinu shirikishi. Mbinu hizi zitamfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji na mwalimu akibaki kuwa mwezeshaji. Aidha, ufundishaji na ujifunzaji wa maudhui yanayolenga kumwezesha mwanafunzi kujenga misingi ya kujitegemea, kuwa mbunifu na kutambua fursa zilizopo katika mazingira yake na kuzitumia kutamwezesha kukabiliana na changamoto za kila siku za maisha. Ufundishaji huu unaozingatia kujifunza kwa vitendo kwa kufanya shughuli mbalimbali tofauti na hapo awali ambapo mwalimu alikuwa akifundisha kwa nadharia zaidi huku akiwakaririsha wanafunzi maudhui.

## 2.6 Upimaji wa ujifunzaji

Upimaji ni sehemu muhimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Kupima kumwezesha mwalimu kubaini kufikiwa kwa ujenzi wa umahiri uliokusudiwa. Kupima kutafanyika kwa kutumia zana za aina mbalimbali. Zana hizi zitajumuisha mitihani ya kuandika, hojaji, uchunguzi makini, maswali ya ana kwa ana, mkoba wa kazi na orodha hakiki. Upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi utahusisha upimaji endelevu.

## 3.0 Maudhui ya muhtasari

Maudhui ya muhtasari yamepangwa kwa kila darasa yakihusisha umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za mwanafunzi, vigezo vya upimaji, upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi na idadi ya vipindi kwa kila umahiri mahususi.

## 3.1 Umahiri mkuu

Huu ni uwezo wa kutenda jambo kwa usahihi na kwa ufanisi unaokusudiwa kwa muda fulani. Umahiri mkuu hujengwa na umahiri mahususi ambao nao hujengwa na mwanafunzi kwa kutenda shughuli mbalimbali.

## 3.2 Umahiri mahususi

Huu ni uwezo ambao hujengwa na mwanafunzi kwa kutenda kwa ufanisi shughuli mbalimbali zilizolengwa ndani ya muktadha wa umahiri mkuu.

### 3.3 Shughuli za mwanafunzi

Hivi ni vitendo ambavyo mwanafunzi anapaswa kuvitenda ili kufikia umahiri mahususi uliokusudiwa kwa kuzingatia uwezo na darasa husika.

### 3.4 Vigezo vya upimaji

Hivi ni viwango vya ufanisi wa utendaji wa mwanafunzi ili kufikia umahiri mahususi uliokusudiwa.

### 3.5 Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi

Huu ni upimaji wa kiwango cha ufikiwaji wa vigezo vya upimaji kwa kila shughuli iliyokusudiwa.

### 3.6 Idadi ya vipindi

Haya ni makadirio ya muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za kutenda mwanafunzi. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni dakika 40. Idadi ya vipindi kwa somo hili ni vipindi 2 kwa wiki. Hata hivyo, mapendekezo haya ya idadi ya vipindi yanaweza kubadilika kulingana na mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.

## 4. Maudhui ya Darasa la V

**Jedwali Na. 2: Umahiri utakaojengwa na mwanafunzi katika Darasa la V**

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|
| 1.0 Kuwa nadhifu | 1.1 Kujenga tabia ya usafi wa mwili<br>1.2 Kutunza mavazi katika kudumisha usafi<br>1.3 Kutunza mazingira katika kudumisha makazi safi |
| 2.0 Kumudu mapishi mbalimbali | 2.1 Kutambua kanuni zinazohitajika katika mapishi mbalimbali<br>2.2 Kutayarisha vyakula aina mbalimbali<br>2.3 Kutengeneza vinywaji |
| 3.0 Kusanifu kazi za sanaa | 3.1 Kumudu misingi ya uimbaji na uigizaji.<br>3.2 Kutengeneza picha zenye ujumbe tofauti kwa jamii<br>3.3 Kubuni chapa tofauti za sanaa za ufundi<br>3.4 Kufinyanga maumbo mbalimbali<br>3.5 Kutengeneza vitu kwa kutumia makunzi yanayopatikana katika mazingira |
| 4.0 Kufahamu stadi za ujasiriamali | 4.1 Kujenga utayari wa kujifunza<br>4.2 Kutambua masoko ya bidhaa ndogondogo<br>4.3 Kutambua kanuni za usimamizi wa fedha |

**Jedwali Na. 3: Maudhui ya muhtasari Darasa la V**

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| 1.0 Kuwa nadhifu. | 1.1 Kujenga tabia ya usafi wa mwili. | a) Kueleza utaratibu wa usafishaji wa mwili. | Utaratibu wa kuoga umeelezewa ipasavyo. | Anaeleza utaratibu wa kuoga bila ya kuzingatia utumiaji wa vifaa sahihi na salama. | Anaeleza utaratibu wa kuoga akizingatia utumiaji wa vifaa sahihi bila kujali usalama wa vifaa. | Anaeleza utaratibu wa kuoga ipasavyo akizingatia utumiaji wa vifaa sahihi na salama. | Anaeleza utaratibu wa kuoga ipasavyo akizingatia kutumia vifaa sahihi na salama na kujikausha kwa usahihi. | 5 |
| | | b) Kueleza utaratibu wa usafi wa mwili wakati wa balehe kwa jinsi zote | Utaratibu wa usafi wa mwili wakati wa balehe umeelezwa kwa usahihi. | Anaeleza utaratibu wa usafi wa mwili wakati wa balehe bila kueleza utumiaji unaofaa wa vifaa vinavyotumika wakati wa balehe | Anaeleza utaratibu wa usafi wa mwili wakati wa balehe na unaofaa sahihi wa vifaa vinavyotumika wakati wa balehe | Anaeleza utaratibu wa usafi wa mwili wakati wa balehe kwa kuzingatia utumiaji na utunzaji unaofaa wa vifaa vinavyotumika wakati wa balehe | Anaeleza utaratibu wa usafi wa mwili wakati wa balehe kwa kuzingatia utumiaji na utunzaji unaofaa wa vifaa pamoja na jinsi ya kutekeleza vilivyotumika | |
| | | c) Kuvaa sare ya shule kwa kufuata utaratibu uliopangwa | Sare ya shule imevaliwa kwa kufuata utaratibu uliopangwa. | Anavaa sare ya shule lakini viatu na soksi siyo vilivyo pendekezwa | Anavaa sare ya shule iliyopendekezwa ila sio nadhifu. | Anavaa sare ya shule iliyo pendekezwa na kwa unadhifu. | Anavaa sare ya shule iliyopendekezwa kwa unadhifu akizingatia kung’arisha viatu vyake | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | 1.2 Kutunza mavazi katika kudumisha usafi | a) Kushona mishono sahili. | Mishono sahili ya kushikiza, kuunga, kupamba na kupinda imeshonwa kwa usahihi | Anashona mshono mmoja kati ya mishono sahili ya kushikiza, kuunga, kupamba na kupinda | Anashona mishono miwili kati ya mishono sahili ya kushikiza, kuunga, kupamba na kupinda. | Anashona mishono sahili ya kushikiza, kuunga, kupamba na kupinda | Anashona mishono yote na kuibainisha kwa kuiandika | 5 |
| | | b) Kurekebisha mavazi yaliyochanika kwa kuzingatia kanuni za urekebishaji wa mavazi | Mavazi yaliyochanika yamerekebishwa kwa usahihi | Anarekebisha vazi lililochanika bila ya kuzingatia kanuni za urekebishaji wa nguo | Anarekebisha vazi lililochanika kwa kuzingatia kanuni za urekebishaji wa nguo bila kufuata utaratibu husika | Anarekebisha vazi lililochanika kwa kuzingatia kanuni za urekebishaji wa nguo | Anarekebisha vazi lililochanika kwa kuzingatia kanuni za urekebishaji wa nguo na kuwaelekeza wenzake | |
| | | c) Kushonea vifungo | Vifungo vimeshonewa kwa ufanisi kwa kufuata kanuni za ushoneaji wa vifungo | Anashonea vifungo bila ya kuzingatia kanuni za ushoneaji wa vifungo | Anashonea vifungo kwa kuzingatia baadhi ya kanuni za ushoneaji | Anashonea vifungo kwa kuzingatia kanuni zote za ushoneaji wa vifungo | Anashonea vifungo kwa kuzingatia kanuni zote za ushoneaji vifungo na kuwaelekeza wenzake | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | 1.3 Kutunza mazingira katika kudumisha makazi safi | a) Kusafisha sakafu kwa kufuata utaratibu | Sakafu imesafishwa kwa kutumia vifaa sahihi na kwa kufuata utaratibu unaotakiwa | Anasafisha sakafu bila ya kutumia vifaa sahihi na hafuati utaratibu unaotakiwa | Anasafisha sakafu kwa kutumia aidha vifaa sahihi au kufuata utaratibu unaotakiwa. | Anasafisha sakafu kwa kutumia vifaa sahihi na kufuata utaratibu unaotakiwa | Anasafisha sakafu kwa kutumia vifaa sahihi, kufuata utaratibu unaotakiwa na kuwaelekeza wenzake | 5 |
| | | b) Kuelezea jinsi ya kufanya usafi sehemu ya kulala. | Uelezaji wa usafishaji wa sehemu ya kulala umefanyika kwa usahihi. | Anaeleza namna ya kufanya usafi wa sehemu ya kulala kwa kila siku tu bila ya kuzingatia usafi wa wiki na maalum | Anaeleza namna ya kusafisha sehemu ya kulala kwa kila siku na aidha kwa wiki au maalumu. | Anaeleza namna ya kufanya usafi wa sehemu ya kulala kwa kila siku, wiki na maalumu | Anaeleza namna ya kufanya usafi sehemu ya kulala kwa kila siku, wiki, maalumu na kupamba chumba | |
| | | c) Kueleza utaratibu wa kuhifadhi taka | Utaratibu wa kuhifadhi taka umeelezewa kwa usahihi | Anaeleza utaratibu wa kuhifadhi taka katika chombo maalumu bila kuzingatia kuzitenganisha na kuzifunika | Anaeleza utaratibu wa kuhifadhi taka katika chombo maalumu akizingatia kuzitenganisha au kuzifunika | Anaeleza utaratibu wa kuhifadhi taka katika chombo maalumu akizingatia kuzitenganisha na kuzifunika | Anaeleza utaratibu wa kuhifadhi taka katika chombo maalumu akizingatia kuzitenganisha, kuzifunika na kutoa maelezo | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| 2.0 Kumudu mapishi tofauti | 2.1 Kutambua kanuni zinazohitajika katika mapishi mbalimbali | a) Kueleza kanuni za usafi binafsi wakati wa kuandaa chakula | Kanuni za usafi binafsi wakati wa kuandaa chakula zimeelezwa kwa usahihi | Anaeleza kanuni moja tu ya usafi binafsi wakati wa kuandaa chakula | Anaeleza kanuni chache za usafi binafsi wakati wa kuandaa chakula | Anaeleza kanuni zote za usafi binafsi wakati wa kuandaa chakula ipasavyo | Anaeleza kanuni zote za usafi binafsi wakati wa kuandaa chakula na kutoa mifano halisi | 5 |
| | | b) Kufanya usafi wa mazigira katika eneo la kuandaa chakula | Usafi wa mazingira wa eneo la kuandaa chakula umefanyika kama ilivyokusudiwa | Anafanya usafi wa mazingira katika eneo la kuandaa chakula akizingatia kanuni moja | Anafanya usafi wa mazingira katika eneo la kuandaa chakula akizingatia kanuni chache | Anafanya usafi wa mazingira katika eneo la kuandaa chakula akizingatia kanuni zote husika | Anafanya usafi wa mazingira katika eneo la kuandaa chakula akizingatia kanuni zote husika na kusafisha vifaa vilivyotumika | |
| | | c) Kubainisha njia tofauti za mapishi ya vyakula | Njia nne tofauti za mapishi ya vyakula zimebainishwa kwa usahihi | Anabainisha njia mojawapo ya mapishi ya vyakula | Anabainisha njia chache za mapishi ya vyakula | Anabainisha njia zote nne za mapishi ya vyakula na kutoa maelezo mafupi | Anabainisha njia zote nne za mapishi ya vyakula na kueleza namna kila njia inavyofanyika | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | **Utendaji chini ya wastani** | **Utendaji wastani** | **Utendaji mzuri** | **Utendaji mzuri sana** | |
| | 2.2 Kutayarisha vyakula vya aina tofauti | a) Kuchemsha chakula kwa kufuata kanuni husika | Chakula kimecheshwa kama ilivyotarajiwa | Anachemsha chakula bila kufuata kanuni za uchemshaji wa chakula na usafi | Anachemsha chakula akizingatia baadhi ya kanuni za uchemshaji wa chakula | Anachemsha chakula akizingatia kanuni zote za uchemshaji wa chakula. na kuzingatia usafi | Anachemsha chakula akizingatia kanuni zote za uchemshaji wa chakula, usafi na kuwaelekeza wenzake | 5 |
| | | b) Kukaanga vyakula kwa mafuta kidogo | Vyakula vimekaangwa kwa usahihi kwa kutumia kiasi sahihi cha mafuta | Anakaanga chakula kwa kutumia kiasi cha mafuta kisichopaswa | Anakaanga chakula kwa kiasi kinachopaswa cha mafuta lakini hakina mwonekano uliotarajiwa | Anakaanga chakula kwa kiasi kinachohitajika cha mafuta na kuwa na mwonekano uliotarajiwa | Anakaanga chakula kwa kiasi kinachopaswa cha mafuta, kuwa na mwonekano uliotarajiwa na kuwaelekeza wenzake | |
| | | c) Kutayarisha vyakula kwa njia ya kuchoma | Vyakula vimetayarishwa kwa njia ya kuchoma kama inavyotakiwa | Anatayarisha chakula kwa njia ya kuchoma bila kufuata utaratibu na usafi | Anatayarisha chakula kwa njia ya kuchoma akifuata utaratibu bila kujali usafi | Anatayarisha chakula kwa njia ya kuchoma akifuata utaratibu unaotakiwa, na kujali usafi | Anatayarisha chakula kwa njia ya kuchoma akifuata utaratibu unaotakiwa, na kujali usafi na kuwaelekeza wenzake | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | 2.3 Kutengeneza vinywaji | a) Kuandaa chai ya maziwa | Chai ya maziwa imeandaliwa kama ilivyotarajiwa | Anaandaa chai ya maziwa bila kuzingatia usafi, viamba upishi sahihi na hakufuata hatua stahiki | Anaandaa chai ya maziwa akizingatia usafi, viamba upishi sahihi lakini hakufuata hatua zinazotakiwa | Anaandaa chai ya maziwa akizingatia usafi, viamba upishi sahihi na kufuata hatua zinazotakiwa | Anaandaa chai ya maziwa akizingatia usafi, viamba upishi sahihi na kufuata hatua zinazotakiwa na kuelekeza wenzake | 5 |
| | | b) Kupika uji | Uji umepikwa kwa usahihi kwa kufuata hatua za kupika uji | Anapika uji bila ya kuzingatia usafi, viamba upishi sahihi na kutofuata hatua zinazotakiwa | Anapika uji akizingatia usafi, viamba upishi sahihi bila kufuata hatua zinazotakiwa | Anapika uji akizingatia usafi, viamba sahihi na kufuata hatua zinazotakiwa | Anapika uji akizingatia usafi, viamba upishi sahihi, kufuata hatua zinazotakiwa na kuwaelekeza wenzake | |
| | | c) Kuandaa juisi kwa kukamua matunda | Juisi ya kukamua matunda imeandaliwa kwa usahihi | Anaandaa juisi ya kukamua matunda bila ya kuzingatia ubora wa matunda na usafi | Anaandaa juisi ya kukamua matunda akizingatia ubora wa matunda lakini hakuzingatia usafi | Anaandaa juisi ya kukamua matunda akizingatia ubora wa matunda na usafi | Anaandaa juisi ya kukamua matunda akizingatia viamba upishi sahihi, ubora wa matunda na kuzingatia usafi | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| 3.0 Kusanifu kazi za sanaa | 3.1 Kumudu misingi ya uimbaji na uigizaji | a) Kuimba nyimbo kwa kuongozwa na ala mbalimbali za muziki | Nyimbo za masomo zimeimbwa vizuri darasani kwa kuongozwa na ala za muziki | Anaimba nyimbo za masomo bila ya kufuata ala za muziki | Anaimba nyimbo za masomo kwa kuongozwa na ala chache za muziki | Anaimba nyimbo za masomo kwa kuongozwa na ala mbalimbali za muziki kama inavyotakiwa | Anaimba nyimbo za masomo kwa kuongozwa na ala mbalimbali za muziki kwa usahihi na kuwasaidia wenzake | 9 |
| | | b) Kuimba nyimbo mbalimbali za kitaifa kwa kuongozwa na mkong'osio wa bendi ya shule | Nyimbo mbalimbali za kitaifa zimeimbwa kwa ustadi mzuri kwa kuongozwa na mkong'osio wa bendi ya shule | Anaimba nyimbo za kitaifa bila ya kufuata mkong'osio wa bendi ya shule | Anaimba nyimbo chache za kitaifa alizopewa kwa kuongozwa na mkong'osio wa bendi ya shule | Anaimba nyimbo zote za kitaifa alizopewa akiongozwa na mkong'osio wa bendi ya shule | Anaimba nyimbo zote za kitaifa alizopewa na zingine akiongozwa na mkong'osio wa bendi ya shule | |
| | | c) Kughani shairi la kimapokeo lenye beti nne kwa ghani tofauti | Shairi la kimapokeo lenye beti nne limeghaniwa kwa ghani tofauti | Anaghani shairi la kimapokeo lenye beti nne kwa ghani moja | Anaghani shairi lenye beti nne la kimapokeo kwa ghani chache | Anaghani shairi la kimapokeo lenye beti nne kwa ghani tofauti na kutoa maelezo | Anaghani shairi lenye beti nne la kimapokeo kwa ghani tofauti na kuongeza nakshi | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | | d) Kuandaa mapambo tofauti ya mchezo wa kuigiza kulingana na ujumbe unaohusika | Mapambo tofauti ya mchezo wa kuigiza yameandaliwa kulingana na ujumbe unaohusika | Anaandaa pambo moja la mchezo wa kuigiza kulingana na ujumbe unaohusika | Anaandaa mapambo machache ya mchezo wa kuigiza kulingana na ujumbe unaohusika | Anaandaa mapambo tofauti ya mchezo wa kuigiza kulingana na ujumbe unaohusika na kutoa ufafanuzi | Anaandaa mapambo toafauti ya mchezo wa kuigiza kulingana na ujumbe unaohusika na kuweka ubunifu | |
| | | e) Kuigiza maigizo tofauti na kueleza ujumbe wake | Maigizo tofauti yameigizwa na kuelezewa ujumbe wake kwa usahihi | Anaigiza igizo bila ya kuelezea ujumbe wake | Anaigiza igizo na kueleza ujumbe wake lakini sio kwa ufasaha | Anaigiza igizo na kueleza ujumbe wake kwa ufasaha | Anaigiza kwa ubunifu mkubwa igizo na kueleza ujumbe wake kwa ufasaha | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | 3.2 Kutengeneza picha zenye ujumbe tofauti kwa jamii | a) Kuchora picha ya njiti yenye watu walio katika mikao tofauti kwa penseli | Picha ya njiti yenye watu walio katika mikao tofauti imechorwa vizuri kwa penseli | Anachora picha ya njiti yenye mtu aliyekaa katika mkao mmoja kwa penseli | Anachora picha ya njiti yenye watu walio katika mikao michache tofauti kwa kutumia penseli | Anachora picha ya njiti yenye watu walio katika mikao tofauti aliyopewa kwa kutumia penseli na kuelezea | Anachora picha ya njiti yenye watu walio katika mikao tofauti aliyopewa kwa kutumia penseli na kuongeza ubunifu | 4 |
| | | b) Kuchora picha za njiti za vitu tofauti kwa penseli | Picha ya njiti yenye vitu tofauti zimechorwa kwa penseli vizuri | Anachora picha ya njiti yenye kitu kimoja kwa penseli | Anachora picha ya njiti yenye vitu vichache vya aina tofauti kwa penseli | Anachora picha ya njiti yenye vitu vingi vya aina tofauti kwa penseli na kuelezea | Anachora picha ya njiti yenye vitu vingi vya aina tofauti kwa penseli na kuongeza ubunifu | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | | c) Kuchora picha ya njiti yenye mchanganyiko wa watu na vitu katika mikao tofauti kwa kutumia penseli | Picha ya njiti yenye mchanganyiko wa watu na vitu katika mikao tofauti zimechorwa kwa usahihi | Anachora picha ya njiti yenye mchanganyiko wa watu na vitu katika mkao mmoja tu | Anachora picha ya njiti yenye mchanganyiko wa watu na vitu katika mikao michache tofauti, kwa kutumia penseli | Anachora picha ya njiti yenye mchanganyiko wa watu na vitu katika mikao mingi tofauti. kwa kutumia penseli | Anachora picha ya njiti yenye mchanganyiko wa watu na vitu katika mikao mingi tofauti kwa kutumia penseli na kuongeza ubunifu | |
| | 3.3 Kubuni chapa tofauti za sanaa za ufundi. | a) Kubaini motifu za aina tofauti zinazofaa kuchapa kutoka kwenye mazingira | Motifu za aina tofauti zinazofaa kuchapa kutoka kwenye mazingira zimebainishwa | Anabaini motifu ya aina moja inayofaa kuchapa kutoka kwenye mazingira | Anabaini aina chache za motifu zinazofaa kuchapa kutoka kwenye mazingira | Anabaini aina nyingi za motifu zinazofaa kuchapa kutoka kwenye mazingira | Anabaini aina nyingi za motifu zinazofaa kuchapa kutoka kwenye mazingira na kuelezea matumizi yake | 4 |
| | | b) Kuandaa vifaa tofauti vya kuchapa | Vifaa tofauti vya kuchapa vimeandaliwa kikamilifu | Anaandaa kifaa kimoja cha kuchapa | Anaandaa vifaa vichache vya kuchapa vilivyoelekezwa | Anaandaa vifaa vingi tofauti vya kuchapa kama ilivyoelekezwa | Anaandaa vifaa vingi tofauti vya kuchapa kama ilivyoelekezwa na kuelezea kazi zake | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | | c) Kuchapa pambo lenye motifu za rangi tofauti kwa kugandamiza | Pambo la motifu za rangi tofauti limechapwa kwa kugandamiza kwa usahihi | Anachapa pambo lenye motifu ya rangi moja kwa kugandamiza kama ilivyokusudiwa | Anachapa pambo lenye motifu za rangi chache kwa kukandamiza | Anachapa pambo lenye motifu za rangi tofauti kwa kukandamiza kwa usahihi kama ilivyokusudiwa | Anachapa pambo lenye motifu za rangi tofauti kwa kukandamiza na kwa ubunifu zaidi | |
| | 3.4 Kufinyanga maumbo tofauti tofauti | a) Kufinyanga maumbo kwa njia ya kufinyafinya | Ufinyanzi wa maumbo tofauti kwa njia ya kufinyafinya kuonyesha sehemu muhimu umefanyika | Anafinyanga umbo moja kwa njia ya kufinyafinya | Anafinyanga maumbo machache kwa njia ya kufinyafinya | Anafinyanga maumbo mengi tofauti kwa njia ya kufinyafinya, kuonesha sehemu muhimu na kutoa maelezo | Anafinyanga maumbo tofauti kwa njia ya kufinyafinya akionesha sehemu muhimu na kuongeza urembo zaidi | 5 |
| | | b) Kufinyanga kifani kwa njia ya bapa. | Ufinyanzi kwa njia ya bapa na kuonesha sehemu muhimu za kifani. | Anafinyanga kifani kwa kubahatisha. | Anafinyanga kifani kwa njia ya bapa lakini hakuonesha sehemu muhimu. | Anafinyanga kifani kwa njia ya bapa na kuonesha sehemu muhimu za kifani na kutoa maelezo | Anafinyanga kifani kwa njia ya bapa akionesha sehemu muhimu za kifani, kuweka nakshi na kueleza wengine | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | | c) Kufinyanga kifani kwa njia ya pindi na kuonesha sehemu muhimu za kifani | Ufinyanzi kwa njia ya pindi umefanyika kwa usahihi na kuonesha sehemu muhimu za kifani | Anafinyanga kifani lakini sio kwa njia ya pindi | Anafinyanga kifani kwa njia ya pindi lakini hakuonesha sehemu muhimu | Anafinyanga kifani kwa njia ya pindi na kuonesha sehemu zake muhimu kwa uhakika | Anafinyanga kifani kwa njia ya pindi na kuonesha sehemu muhimu za kifani na kuongeza ubunifu | |
| | | d) Kukausha kifani cha udongo kwa kufuata hatua zote | Ukaushaji wa kifani cha udongo kwa kufuata hatua zote umefanyika kwa usahihi | Amekausha kifani cha udongo bila ya kufuata hatua zinazotakiwa | Anakausha kifani cha udongo kwa kufuata hatua chache zinazotakiwa | Anakausha kifani cha udongo kwa kufuata hatua zote zinazotakiwa kwa uhakika na kujiamini | Anakausha kifani cha udongo kwa kufuata hatua zote zinazotakiwa na kuongeza urembo au nakshi | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | **Utendaji chini ya wastani** | **Utendaji wastani** | **Utendaji mzuri** | **Utendaji mzuri sana** | |
| | 3.5 Kutengeneza vitu tofauti kwa kutumia makunzi yanayopatikana katika mazingira | a) Kusuka kili tofauti kwa njia tofauti | Kili tofauti zimesukwa kwa njia tofauti kwa usahihi | Anasuka kili kwa njia moja tu na ameshindwa kueleza | Anasuka kili chache kwa njia tofauti | Anasuka kili nyingi kwa njia tofauti na kueleza hatua zake | Anasuka kili nyingi kwa njia tofauti kwa usahihi na kuongeza urembo | 5 |
| | | b) Kusokota kamba kwa njia tofauti | Kamba zimesokotwa kwa njia tofauti kwa usahihi | Anasokota kamba kwa njia moja | Anasokota kamba kwa njia chache tofauti | Anasokota kamba kwa njia nyingi kwa uhakika na kueleza | Anasokota kamba kwa njia nyingi na kuongeza urembo | |
| | | c) Kutengeneza vitu tofauti kwa kutumia kili/kamba iliyosokotwa | Vitu tofauti vimetengenezwa kwa kutumia kili au kamba iliyosokotwa kwa usahihi | Anatengeneza kitu cha aina moja kwa kutumia kili/ kamba iliyosokotwa | Anatengeneza vitu vichache tofauti kwa kutumia kili/kamba iliyosokotwa | Anatengeneza vitu vingi tofauti kwa kutumia kili/kamba iliyosokotwa | Anatengeneza vitu vingi tofauti kwa kutumia kili/kamba iliyosokotwa na kuongeza nakshi | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| 4.0 Kufahamu stadi za ujasiriamali | 4.1 Kujenga utayari wa kujifunza | a) Kusikiliza maelekezo kwa makini na kuyatekeleza | Maelekezo yamesikilizwa na kutekelezwa kama ilivyotarajiwa | Anasikiliza maelekezo lakini hatekelezi chochote | Anatekeleza maelekezo kwa kiwango kidogo | Anatekeleza maelekezo kwa makini kama ilivyotarajiwa | Anatekeleza maelekezo kwa makini kama ilivyotarajiwa kwa kiwango kikubwa | 5 |
| | | b) Kudadisi ili kujenga maarifa katika kujifunza | Udadisi umefanyika ili kujenga maarifa katika kujifunza | Anadadisi bila mpangilio ili kujenga maarifa katika kujifunza | Anadadisi kwa mpangilio ili kujenga maarifa katika kujifunza | Anadadisi kwa kutumia maswali tofauti ili kujenga maarifa katika kujifunza | Anadadisi kwa kutumia maswali tofauti yenye kufikiri kiyakinifu ili kujenga maarifa katika kujifunza | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | | c) Kujiunga katika klabu tofauti za masomo ili kuibua stadi muhimu za kujifunza | Klabu tofauti ya somo imesaidia kuibua stadi muhimu za kujifunza | Anajiunga katika klabu ya somo lakini hadadisi mambo mbalimbali ili kuibua stadi muhimu za kujifunza | Anajiunga katika klabu ya somo akidadisi mambo mbalimbali ili kuibua stadi muhimu za kujifunza | Anajiunga katika klabu ya somo akidadisi mambo mbalimbali kiyakinifu ili kuibua stadi muhimu za kujifunza | Anajiunga katika klabu ya somo akidadisi mambo mbalimbali kiyakinifu na kuwaelewesha wenzake ili kuibua stadi muhimu za kujifunza na kuwashawishi wenzake kujiunga | |
| | 4.2 Kutambua masoko ya bidhaa ndogo ndogo | a) Kubaini aina tofauti za bidhaa zinazohitajika kulingana na nyakati katika soko | Bidhaa tofauti zinazohitajika sokoni kulingana na nyakati zimebainishwa kwa usahihi | Anabainisha aina moja ya bidhaa inayohitajika kulingana na nyakati katika soko | Anabainisha aina chache za bidhaa zinazohitajika kulingana na nyakati katika soko | Anabainisha aina nyingi za bidhaa zinazohitajika kulingana na nyakati za soko na kueleza kwa ufasaha | Anabainisha aina nyingi za bidhaa zinazohitajika kulingana na nyakati katika soko kwa usahihi na kupendekeza bei zake | 9 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | | b) Kubaini viwango vya gharama za bidhaa tofauti kulingana na hali ya uzalishaji wa bidhaa | Viwango vya gharama za bidhaa kulingana na hali ya uzalishaji zimebainishwa kama ilivyotarajiwa | Anabainisha kiwango cha bidhaa moja kulingana na hali ya uzalishaji | Anabainisha viwango vya gharama za bidhaa chache kulingana na hali ya uzalishaji wa bidhaa | Anabainisha viwango vya gharama za bidhaa nyingi kulingana na hali ya uzalishaji wa bidhaa | Anabainisha viwango vya gharama za bidhaa nyingi kulingana na hali ya uzalishaji wa bidhaa na kuelezea sababu zake | |
| | | c) Kupanga bei za bidhaa kulingana na bei iliyoko sokoni | Bei za bidhaa tofauti zimepangwa kwa usahihi kulingana na bei zilizoko sokoni | Anapanga bei ya bidhaa moja kulingana na bei iliyopo sokoni | Anapanga bei za bidhaa chache kulingana na bei iliyopo sokoni | Anapanga bei ya bidhaa nyingi kulingana na bei iliyopo sokoni | Anapanga bei ya bidhaa nyingi kulingana na bei iliyopo sokoni na kuweka katika mpangilio mzuri katika daftari lake | |
| | | d) Kueleza faida ya kujua muda wa uhai wa bidhaa | Faida za kujua uhai wa muda wa bidhaa umeelezewa vizuri | Anaeleza faida moja ya kujua muda wa uhai wa bidhaa | Anaeleza faida chache za kujua muda wa uhai wa bidhaa | Anaeleza faida nyingi za kujua muda wa uhai wa bidhaa | Anaeleza faida nyingi za kujua muda wa uhai wa bidhaa na kuongeza maelezo mengine | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | | e) Kubainisha tofauti iliyopo kati ya duka na soko ili kujua ni aina gani ya bidhaa zinahitajika katika sehemu husika | Tofauti kati ya duka na soko imebainishwa kwa usahihi ili kujua ni aina gani ya bidhaa inahitajika | Anabainisha bidhaa za duka na soko kwa kubahatisha | Amebainisha bidhaa zinazohitajika dukani na sokoni kama ipasavyo | Anabainisha tofauti kati ya duka na soko na kujua aina ya bidhaa zinahitajika katika sehemu zote mbili na kutoa maelezo | Anabainisha tofauti kati ya duka na soko akiorodhesha aina ya bidhaa zinahitajika katika sehemu zote mbili na kupanga bei zake | |
| | 4.3 Kutambua taratibu za usimamizi wa fedha | a) Kutunza kumbukumbu tofauti za mapato na matumizi ya fedha | Kumbukumbu za matumizi na mapato ya fedha zimetunzwa kama ilivyotarajiwa | Anatunza kumbukumbu za mapato au matumizi ya fedha tu | Anatunza kumbukumbu za mapato ya fedha na matumizi yake | Anatunza kumbukumbu za mapato na matumizi ya fedha na kutoa maelezo | Anatunza kumbukumbu za mapato na matumizi ya fedha katika mpangilio mzuri na kuwaelekeza wenzake | 5 |
| | | b) Kubaini njia tofauti za kuhifadhi fedha (akiba) | Njia tofauti za kuhifadhi fedha (akiba) zimebainishwa kwa usahihi | Anabaini njia moja ya kuhifadhi fedha | Anabaini njia chache za kuhifadhi fedha (akiba) | Anabaini njia nyingi za kuhifadhi fedha (akiba) na kuelezea kutokana na muktadha | Anabaini njia nyingi za kuhifadhi fedha (akiba) kwa usahihi na kueleza faida halisi za kila njia | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | | c) Kutambua huduma tofauti za kifedha zinazotolewa kwa njia ya simu | Huduma tofauti za kifedha zinazotolewa kwa njia ya simu zimebainishwa | Anabainisha huduma moja ya kifedha inayotolewa kwa njia ya simu | Anabainisha huduma chache za kifedha zinazotolewa kwa njia ya simu | Anabainisha huduma nyingi za kifedha zinazotolewa kwa njia ya simu kwa usahihi | Anabainisha huduma nyingi za kifedha zinazotolewa kwa njia ya simu na kueleza faida zake | |

## 5. Maudhui ya Darasa la VI

**Jedwali la 4: Umahiri utakaojengwa na mwanafunzi katika Darasa la Sita**

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|
| 1.0 Kuwa nadhifu | 1.1 Kutunza mavazi katika kudumisha usafi<br>1.2 Kutunza mazingira katika kudumisha makazi safi |
| 2.0 Kumudu mapishi mbalimbali | 2.1 Kutayarisha vyakula vya aina tofauti<br>2.2 Kutengeneza vinywaji<br>2.3 Kujenga nidhamu ya utumiaji wa meza wakati wa kula |
| 3.0 Kusanifu kazi za sanaa | 3.1 Kumudu uimbaji na uigizaji<br>3.2 Kutengeneza picha zenye ujumbe tofauti kwa jamii<br>3.3 Kubuni chapa tofauti za sanaa za ufundi.<br>3.4 Kufinyanga maumbo tofauti tofauti<br>3.5 Kutengeneza vitu kwa kutumia makunzi yanayo patikana katika mazingira |
| 4.0 Kufahamu stadi za ujasiriamali | 4.1 Kujenga utayari wa kujifunza<br>4.2 Kutambua masoko ya bidhaa ndogondogo<br>4.3 Kutambua kanuni za usimamizi wa fedha |

**Jedwali la 5: Maudhui ya muhtasari Darasa la VI**

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| 1.0 Kuwa nadhifu | 1.1 Kutunza mavazi katika kudumisha usafi | a) Kufua nguo | Nguo zimefuliwa kwa usahihi kwa kufuata hatua za ufuaji nguo | Anafua nguo kwa kufuata hatua moja ya ufuaji nguo | Anafua nguo kwa kuzingatia hatua chache za ufuaji nguo | Anafua nguo kwa kuzingatia hatua zote za ufuaji nguo | Anafua nguo kwa usahihi kwa kuzingatia hatua zote za ufuaji nguo na kuwaelekeza wenzake | 6 |
| | | b) Kupiga nguo pasi | Nguo zimepingwa pasi kwa usahihi kwa kuzingatia hatua zinazotakiwa | Anapiga nguo pasi akizingatia hatua moja tu kati ya zinazotakiwa | Anapiga nguo pasi akizingatia hatua chache zinazotakiwa | Anapiga nguo pasi akizingatia hatua zote zinazotakiwa | Anapiga nguo pasi akizingatia hatua zote zinazotakiwa na kuzihifadhi vizuri | |
| | | c) Kusafisha viatu | Viatu vimesafishwa kwa usahihi kulingana na aina ya viatu | Anasafisha viatu lakini hakutumia vifaa sahihi | Anasafisha viatu kwa kutumia vifaa sahihi lakini hakujali kuvisafisha ndani | Anasafisha viatu kwa usahihi ndani na nje kwa kutumia vifaa sahihi | Anasafisha viatu kwa usahihi ndani na nje kwa kutumia vifaa sahihi na kuving’arisha kwa rangi husika | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | 1.2 Kutunza mazingira katika kudumisha makazi safi | a) Kutunza bustani | Bustani zimetunzwa vizuri kwa kuzingatia utaratibu unaotakiwa | Anatunza bustani kwa kuzingatia utaratibu mmoja tu:<br>-kupalilia,<br>-kuweka maji, au<br>-kuweka mbolea | Anatunza bustani akizingatia kumwagilia na kupalilia bila ya kuzingatia kuweka mbolea | Anatunza bustani akizingatia taratibu zote zinazotakiwa na kutoa maelezo | Anatunza bustani akizingatia taratibu zote zinazotakiwa na kuongeza mambo mengine | 6 |
| | | b) Kufukia taka zinazooza | Taka zinazooza zimefukiwa kwa utaratibu unaotakiwa | Anafukia taka zinazooza bila ya kuzingatia utaratibu unaotakiwa | Anafukia taka akizingatia baadhi ya taratibu zinazotakiwa | Anafukia taka akizingatia taratibu zote zinazotakiwa | Anafukia taka akizingatia taratibu zote zinazotakiwa na kutoa maelezo | |
| | | c) Kuhifadhi takataka zisizooza. | Takataka zisizooza zimehifadhiwa kwa utaratibu unaotakiwa | Anahifadhi takataka zisizooza bila ya kufuata utaratibu wowote | Anahifadhi takataka zisizooza akizingatia baadhi ya taratibu zinazotakiwa | Anahifadhi takataka zisizooza akizingatia taratibu zote zinazotakiwa | Anahifadhi takataka zisizooza akizingatia taratibu zote zinazotakiwa na kutoa maelezo | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| 2.0 Kumudu mapishi mbalimbali. | 2.1 Kutayarisha vyakula vya aina tofauti. | a) Kukaanga vyakula tofauti vina vyokaangwa kwa mafuta mengi kwa kuzingatia taratibu zinazotakiwa | Vyakula vimekaangwa katika mafuta mengi kwa kufuata taratibu zinazotakiwa | Anakaanga chakula katika mafuta mengi bila ya kufuata taratibu zozote | Anakaanga chakula katika mafuta mengi akifuata baadhi ya taratibu zinazotakiwa | Anakaanga chakula katika mafuta mengi akifuata taratibu zote zinazotakiwa | Anakaanga chakula katika mafuta mengi akifuata taratibu zote zinazotakiwa na kuelezea wenzake aliyojifunza | 6 |
| | | b) Kuandaa vyakula vya safari | Vyakula vya safari vimeandaliwa kwa kuzingatia taratibu zinazotakiwa | Anaandaa chakula cha safari bila ya kuzingatia utaratibu wowote | Anaandaa chakula cha safari kwa kuzingatia baadhi ya taratibu zinazotakiwa | Anaandaa chakula cha safari kwa kuzingatia taratibu zote zinazotakiwa | Anaandaa chakula cha safari kwa kuzingatia taratibu zote zinazotakiwa na kutoa maelezo | |
| | | c) Kufungasha vyakula kwa njia tofauti | Vyakula vimefungashwa kwa kuzingatia taratibu zinazotakiwa | Anafungasha chakula bila ya kuzingatia utaratibu wowote | Anafungasha chakula akizingatia baadhi ya taratibu zinazotakiwa | Anafungasha chakula akizingatia taratibu zote zinazotakiwa | Anafungasha chakula akizingatia taratibu zote zinazotakiwa na kuwasaidia wenzake | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | **Utendaji chini ya wastani** | **Utendaji wastani** | **Utendaji mzuri** | **Utendaji mzuri sana** | |
| | 2.2 Kutengeneza vinywaji vya aina mbalimbali | a) Kuandaa juisi kwa kupondaponda matunda | Juisi ya kupondaponda matunda imeandaliwa kwa usahihi | Anaandaa juisi kwa kuponda ponda matunda bila ya kuzingatia ubora wa matunda na usafi | Anaandaa juisi kwa kupondaponda matunda akizingatia ubora wa matunda lakini bila kujali usafi | Anaandaa juisi kwa kupondaponda matunda kwa kuzingatia ubora wa matunda na usafi | Anaandaa juisi kwa kupondaponda matunda kwa kuzingatia ubora wa viamba upishi na kueleza sababu | 4 |
| | | b) Kuanda juisi kwa njia ya kuloweka viambaupishi husika | Juisi imeandaliwa kwa njia ya kuloweka kwa usahihi kama ilivyotarajiwa | Anaandaa viambaupishi tu | Anaandaa juisi kwa njia ya kuloweka viambaupishi bila ya kuzingatia ubora wake na vipimo | Anaandaa juisi kwa njia ya kuloweka viambaupishi akizingatia ubora wake na kiasi cha vipimo | Anaandaa juisi kwa njia ya kuloweka viambaupishi akizingatia ubora wake na kiasi cha vipimo na kuwaelekeza wenzake | |
| | 2.3 Kujenga stadi zinazohitajika wakati wa kula | a) Kutenga chakula mezani | Chakula kimetengwa mezani kwa kuzingatia taratibu zinazotakiwa | Anatenga chakula mezani bila ya kuzingatia utaratibu wowote | Anatenga chakula mezani akizingati baadhi ya taratibu zinazotakiwa | Anatenga chakula mezani akizingatia taratibu zote zinazotakiwa | Anatenga chakula mezani akizingatia taratibu zote zinazotakiwa na kuwaelekeza wenzake | 6 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | | b) Kueleze utaratibu wa kuzingatiwa wakati wa kula chakula | Utaratibu wa kuzingatiwa wakati wa kula umeelezewa ipasavyo | Anaeleza utaratibu mmoja tu wa kuzingatia wakati wa kula chakula | Anaelezea taratibu chache za kuzingatiwa wakati wa kula chakula | Anaelezea taratibu zote za kuzingatiwa wakati wa kula chakula | Anaelezea taratibu zote za kuzingatiwa wakati wa kula chakula na kutoa ufafanuzi | |
| | | c) Kuanua meza baada ya kula chakula | Meza imesafishwa kwa utaratibu unaotakiwa | Anaanua meza bila ya kuzingatia taratibu zinazotakiwa | Anaanua meza kwa kuzingatia baadhi ya taratibu | Anaanua meza kwa kuzingatia taratibu zote | Anaanua meza kwa kuzingatia taratibu zote na kutoa maelezo | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | **Utendaji chini ya wastani** | **Utendaji wastani** | **Utendaji mzuri** | **Utendaji mzuri sana** | |
| 3.0 Kusanifu kazi za sanaa | 3.1 Kumudu misingi ya uimbaji na uigizaji | a) Kubainisha makundi ya ala za muziki kwa usahihi | Ala za muziki zimebainishwa kwa usahihi kulingana na makundi yake | Anabainisha kundi moja tu la ala za muziki | Anabainisha baadhi ya makundi ya ala za muziki | Anabainisha makundi yote ya ala za muziki kutoa mifano halisi | Anabainisha makundi yote ya ala za muziki kwa usahihi na kuzitolea maelezo | 10 |
| | | b) Kuandaa mapambo mchezo wa kuigiza kulingana na ujumbe | Mapambo ya mchezo wa kuigiza kulingana na ujumbe yameandaliwa kwa usahihi | Anaandaa makunzi ya mapambo ya mchezo wa kuigiza bila kuzingatia ujumbe | Anaandaa mapambo machache ya mchezo wa kuigiza kwa kuzingatia ujumbe | Anaandaa mapambo mengi ya mchezo wa kuigiza kwa kuzingatia ujumbe na kueleza kwa kifupi | Anaandaa mapambo mengi ya mchezo wa kuigiza kwa kuzingatia ujumbe na kutolea maelezo ya kina kwa ufasaha | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | | c) Kutamba ngonjera kwa kufuata taratibu zinazotakiwa | Ngonjera imetambwa kwa kufuata taratibu zinazotakiwa | Anatamba ngonjera bila ya kuzingatia taratibu zinazotakiwa | Anatamba ngonjera kwa kufuata baadhi ya taratibu zinazotakiwa | Anatamba ngonjera kwa kufuata taratibu zote zinazotakiwa | Anatamba ngonjera kwa kufuata taratibu zote zinazotakiwa na kuongezea madoido | |
| | | d) Kujigamba kwa kutumia wasifu wa vitu, magonjwa, wanyama na ndege waliomo katika mazingira yake | Majigambo yenye wasifu wa vitu, magonjwa, wanyama na ndege waliomo katika mazingira yake yamefanyika kwa kuzingatia taratibu zinazotakiwa | Anajigamba kwa kutumia vitu tofauti vilivyo katika mazingira yake bila ya kuzingatia taratibu zinazotakiwa | Anajigamba kwa kutumia vitu tofauti vilivyo katika mazingira yake akizingatia baadhi ya taratibu zinazotakiwa | Anajigamba kwa kutumia vitu tofauti vilivyo katika mazingira yake akizingatia taratibu zote zinazotakiwa na kutoa mifano halisi | Anajigamba kwa kutumia vitu tofauti vilivyo katika mazingira yake akizingatia taratibu zote zinazotakiwa na kutoa ufafanuzi | |
| | | e) Kuigiza maigizo tofauti kwa njia ya kuganda | Maigizo tofauti kwa njia ya kuganda yamefanyika ipasavyo | Ameigiza igizo moja kwa njia ya mgando | Anaigiza maigizo machache kwa njia ya mgando | Anaigiza maigizo mengi kwa njia ya kuganda kwa ufanisi | Anaigiza maigizo mengi kwa njia ya kuganda kwa ufanisi na kutoa ufafanuzi wa kina | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | 3.2 Kutengeneza picha zenye ujumbe tofauti kwa jamii | a) Kutengeneza picha ya kubandika kwa kuzingatia vigezo vya sanaa | Picha ya kubandika imetengenezwa kwa kuzingatia vigezo vya usanii wa picha | Anatengeneza picha ya kubandika bila ya kuzingatia vigezo | Anatengeneza picha za kubandika akizingatia baadhi ya vigezo vyake | Anatengeneza picha za kubandika akizingatia vigezo vyote vinavyotakiwa | Anatengeneza picha ya kubandika kwa kuzingatia vigezo vyote na kuongeza madoido | 6 |
| | | b) Kuandaa fremu ya picha | Fremu ya picha imeandaliwa kwa kufuata hatua zake | Anaandaa fremu ya picha. bila ya kufuata hatua zinazotakiwa | Anaandaa fremu ya picha. kwa kufuata hatua chache | Anaandaa fremu ya picha kwa kufuata hatua zote na kutoa maelezo | Anaandaa fremu ya picha kwa kufuata hatua zote kwa usahihi na kuongeza mambo mengine | |
| | | c) Kubandika picha yenye kuonesha mizania ya rangi na maumbo | Picha iliyotengenezwa imeonesha mizania ya maumbo na rangi ipasavyo | Anakata maumbo ya picha tu | Anakata na kubandika picha yenye kuonesha mizania ya maumbo bila ya rangi | Anakata na kubandika picha yenye kuonesha mizania ya maumbo na rangi ipasavyo | Anakata na kubandika picha yenye kuonesha mizania ya maumbo na rangi kutoa ufafanuzi wa kina | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | **Utendaji chini ya wastani** | **Utendaji wastani** | **Utendaji mzuri** | **Utendaji mzuri sana** | |
| | 3.3 Kubuni chapa tofauti za sanaa za ufundi. | a) Kuchonga motifu za maumbo ya kijometri kwa kutumia makunzi laini | Motifu za maumbo ya kijometri za makunzi laini zimechongwa ipasavyo | Amechonga motifu moja tu ya umbo la kijometri | Anachonga motifu chache za maumbo ya kijiometri | Anachonga motifu nyingi za maumbo ya kijometri vizuri na kutoa maelezo | Anachonga motifu za maumbo ya kijometri na kuongeza mambo mengine | 6 |
| | | b) Kuchapa ruwaza ya motifu za kijometri kwa rangi za msingi | Ruwaza yenye motifu za kijometri za rangi za msingi imechapwa ipasavyo | Anaandaa vifaa vya kupigia chapa tu | Anachapa ruwaza yenye motifu chache za kijometri kwa rangi za msingi. | Anachapa ruwaza yenye motifu nyingi za kijometri za rangi za msingi ipasavyo | Anachapa ruwaza yenye motifu nyingi za kijometri za rangi za msingi na kuongezea madoido | |
| | | c) Kuweka fremu ya utepe kwenye pambo la ruwaza | Fremu ya utepe imewekwa kwenye pambo la ruwaza kwa usahihi | Anapima na kukata fremu ya utepe wa pambo | Anaweka fremu ya utepe kwenye pambo la ruwaza ila haikuwa na ulinganifu sawasawa pande mbili | Anaweka fremu ya utepe kwenye pambo la ruwaza na imebandikwa sawasawa | Anaweka fremu ya utepe kwenye pambo la ruwaza sawasawa na kuonyesha mambo mengine | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | 3.4 Kufinyanga maumbo tofauti. | a) Kutwanga kinyunya cha karatasi na kukichanganya na gundi ili kuleta ushikamano | Kinyunya cha karatasi kimetwangwa na kuchanganywa na gundi ipasavyo | Anatwanga na kuchanganya kinyunya cha karatasi na gundi kikawa teketeke sana | Anatwanga na kuchanganya kinyunya cha karatasi na gundi kikawa kizito mno | Anatwanga na kuchanganya kinyunya cha karatasi na gundi kikawa na mshikamano upasao | Anatwanga na kuchanganya kinyunya cha karatasi na gundi kikawa na mshikamano upasao na kutoa maelezo | 6 |
| | | b) Kuunda kiunzi cha ndani cha kifani cha mnyama | Uundaji wa kiunzi cha ndani cha kifani cha mnyama umefanywa kikamilifu | Anaunda kiunzi cha ndani cha kifani cha mnyama kisichofungwa imara | Anaunda kiunzi cha ndani cha kifani cha mnyama kilichofungwa imara lakini sio linganifu | Anaunda kiunzi cha ndani cha kifani cha mnyama kilicho imara na linganifu | Anaunda kiunzi cha ndani cha kifani cha mnyama kilicho imara na linganifu chenye umbo kubwa na la kuonekana vizuri sana | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | | c) Kukandika kiunzi cha ndani cha kifani cha mnyama kwa kinyunya cha karatasi na kutia nakshi | Ukandikaji wa kiunzi cha ndani cha kifani cha mnyama kwa kinyunya cha karatasi na kutia nakshi umefanyika ipasavyo | Anaandaa vifaa vya kukandika kiunzi cha ndani cha kifani cha mnyama | Anakandika kiunzi cha ndani cha kifani cha mnyama kwa kinyunya cha karatasi kwa kujaza vizuri na kutia nakshi | Anakandika kiunzi cha ndani cha kifani cha mnyama kwa kinyunya cha karatasi, kukisawazisha na kutia nakshi | Anakandika kiunzi cha ndani cha kifani cha mnyama kwa kinyunya cha karatasi kikamilifu na kukitia nakshi hadi kikawa mororo na kutoa maelezo | |
| | 3.5 Kutengeneza vitu anuwai kwa kutumia makunzi yanayopatikana katika mazingira | a) Kushona kifani cha kili na kukinakshi | Kifani cha kili kimeshonwa na kunakshiwa kama ilivyokusudiwa | Anashona kifani cha kili lakini hawezi kukinakshi | Anashona kifani cha kili na kukinakshi lakini hakuzingatia uwiano wa rangi | Anashona kifani cha kili na kukinakshi akizingatia uwiano wa rangi | Anashona kifani cha kili na kukinakshi kwa usahihi akizingatia uwiano wa rangi na kuzingatia usafi | 6 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | | b) Kutengeneza mapambo kwa kutumia makunzi yanayopatikana katika mazingira yake | Mapambo yametengenezwa kwa usahihi kwa kutumia makunzi yanayopatikana katika mazingira | Anaandaa vifaa vya kutengeneza mapambo kwa kutumia makunzi yanayopatikana katika mazingira yake | Anatengeneza mapambo machache kwa kutumia makunzi yanayopatikana katika mazingira yake na kutoa maelezo mafupi | Anatengeneza mapambo mengi kwa kutumia makunzi yanayopatikana katika mazingira yake na kufafanua | Anatengeneza mapambo mengi kwa kutumia makunzi yanayopatikana katika mazingira yake na kuongeza ubunifu kwa kutumia rangi | |
| | | c) Kutengeneza vifaa kwa kutumia mabaki ya vitu vilivyotumika. | Vifaa vimetengenezwa kwa kutumia mabaki ya vitu vilivyotumika. | Anatengeneza kifaa kimoja kwa kutumia mabaki ya vitu vilivyotumika. | Anatengeneza vifaa vichache kwa kutumia mabaki ya vitu vilivyotumika. | Anatengeneza vifaa vingi kwa kutumia mabaki ya vitu vilivyotumika. | Anatengeneza vifaa vingi kwa kutumia mabaki ya vitu vilivyotumika na kutoa ufafanuzi | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| 4.0 Kufahamu stadi za ujasiriamali | 4.1 Kujenga utayari wa kujifunza | a) Kushiriki katika midahalo mbalimbali ili kupata maarifa | Midahalo mbalimbali imesaidia kuwapatia maarifa | Anashiriki mdahalo kupata maarifa bila kuchangia chochote | Anashiriki midahalo na kutoa hoja chache | Anashiriki midahalo mingi na kuchangia hoja chache kwa mtiririko | Anashiriki midahalo mbalimbali na kuchangia hoja zake kwa mpangilio wa kufikiri kiyakinifu | 4 |
| | | b) Kufanya udadisi wa mambo mbalimbali ili kujenga uwezo wa namna mpya ya kutenda mambo kadhaa | Udadisi wa mambo mbalimbali umefanyika na kuwajengea uwezo wa namna mpya ya kutendwa jambo | Anafanya udadisi wa mambo machache bila ya kujenga uwezo wa namna mpya ya kutenda jambo | Anafanya udadisi wa mambo machache na kujifunza namna mpya ya kutendwa mambo | Anafanya udadisi wa mambo mengi na kujifunza namna mpya ya kutendwa mambo kadhaa | Anafanya udadisi wa mambo mengi na kujifunza namna mpya ya kutendwa na kuelewesha wenzake | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | 4.2 Kutafuta masoko ya bidhaa ndogondogo | a) Kutambua njia bora za ufungashaji wa bidhaa | Njia bora za ufungashaji wa bidhaa zimebainishwa kwa usahihi | Anabainisha njia moja bora ya ufungashaji wa bidhaa | Anabainisha njia bora chache za ufungashaji wa bidhaa | Anabainisha njia bora nyingi za ufungashaji wa bidhaa | Anabainisha njia bora nyingi za ufungashaji wa bidhaa na kuzitolea maelezo kwa ufasaha | 8 |
| | | b) Kubaini aina za wateja kulingana na bidhaa zinazozalishwa | Aina za wateja zimebainishwa kwa usahihi kulingana na bidhaa zinazozalishwa | Anabainisha aina moja ya wateja kulinga na bidhaa bila maelezo | Anabainisha aina chache za wateja kwa kuzingatia bidhaa bila maaelezo yake | Anabainisha aina nyingi za wateja kulingana na bidhaa na kutoa maelezo | Anabainisha aina nyingi za wateja kulingana na bidhaa zinazozalishwa na kutolea ufafanuzi | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | | c) Kubaini udanganyifu unaoweza kufanywa na watu anaoshirikiana nao katika biashara | Udanganyifu wa watu katika kufanya biashara umebainishwa kwa usahihi | Anabainisha udanganyifu kidogo unaofanywa na watu wanaoshirikiana katika kufanya biashara | Anabainisha udanganyifu wa bidhaa chache unaofanywa na watu wanaoshirikiana katika kufanya biashara | Anabainisha udanganyifu wa manunuzi ya bidhaa nyingi unaofanywa na watu wanaoshirikiana katika kufanya biashara | Anabainisha udanganyifu wa bidhaa, manunuzi na fedha bandia unaofanywa na watu wanaoshirikiana katika kufanya biashara | |
| | | d) Kutaja vifaa halali vitumikavyo kupimia bidhaa mbalimbali | Vifaa halali vinavyotumika kupimia bidhaa mbalimbali vimetajwa kwa usahihi | Anataja kifaa kimoja halali kinachotumika kupimia bidhaa. | Anataja vifaa vichache halali vinavyotumika kupimia bidhaa. | Anataja vifaa vingi halali vinavyotumika kupimia bidhaa na kutoa maelezo | Anataja vifaa vingi halali vinavyotumika kupimia bidhaa kwa kutoa mifano halisi. | |
| | 4.3 Kutambua kanuni za usimamizi wa fedha | a) Kutayarisha mizania ya biashara yenye kuzingatia vipengele vyake muhimu | Mizania ya biashara imetayarishwa kwa kuzingatia vipengele vyake muhimu kama ilivyokusudiwa | Anatayarisha mizania ya biashara kwa kuzingatia kipengele kimoja tu | Anatayarisha mizania ya biashara kwa kuzingatia vipengele vichache bila kutoa maelezo | Anatayarisha mizania ya biashara kwa kuzingatia vipengele vingi na kutoa maelezo kwa ufupi | Anatayarisha mizania ya biashara kwa kuzingatia vipengele vingi kwa usahihi na kuongeza mambo mapya | 8 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | | b) Kubaini aina za rejesta zinazotumika kutunza kumbukumbu za bidhaa na fedha | Rejista zitumikazo kutunza kumbukumbu za bidhaa na fedha zimebainishwa kwa usahihi | Anabaini aina moja ya rejesta za kutunza kumbukumbu za bidhaa na fedha kwa usahihi | Anabaini aina chache za rejesta za kutunza kumbukumbu za bidhaa na fedha kwa usahihi | Anabaini aina nyingi za rejesta za kutunza kumbukumbu za bidhaa na fedha kwa kutoa mifano halisi | Anabaini aina nyingi za rejesta za kutunza kumbukumbu za bidhaa na fedha na kufafanua kwa kina | |
| | | c) Kutambua aina nne za kodi zinazotakiwa kulipwa kutokana na bidhaa zinazouzwa | Kodi za aina nne zinazotakiwa kulipwa zimetambuliwa kwa usahihi | Anatambua aina moja ya kodi zinazolipwa kutokana na uuzaji wa bidhaa | Anatambua aina chache za kodi zinazolipwa kutokana na uuzaji wa bidhaa | Anatambua aina nyingi za kodi zinazolipwa kutokana na uuzaji wa bidhaa na kutoa mifano halisi | Anatambua aina nyingi za kodi zinazolipwa kutokana na uuzaji wa bidhaa, kufafanua na kutoa mifano halisi. | |
| | | d) Kupanga bajeti kulingana na mahitaji | Bajeti imepangwa kwa usahihi kulingana na mahitaji | Anapanga bajeti bila ya kuzingatia mahitaji | Anapanga bajeti kulingana na mahitaji bila ya kuainisha vipengele | Anapanga bajeti kulingana na mahitaji na kuainisha vipengele | Anapanga bajeti kulingana na mahitaji akiainisha vipengele na kutoa ufafanuzi kwa ufasaha | |

## 6. Maudhui ya Darasa la VII

**Jedwali la 6: Umahiri utakaojengwa na mwanafunzi katika Darasa la VII**

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|
| 1.0 Kuwa nadhifu | 1.1 Kujenga tabia ya usafi wa mwili<br>1.2 Kutunza mavazi katika kudumisha usafi<br>1.3 Kutunza mazingira katika kudumisha makazi safi |
| 2.0 Kumudu mapishi mbalimbali | 2.1 Kutambua kanuni zinazohitajika katika mapishi<br>2.2 Kutayarisha vyakula aina tofauti<br>2.3 Kutengeneza vinywaji tofauti |
| 3.0 Kusanifu kazi za sanaa | 3.1 Kumudu misingi ya uimbaji na uigizaji<br>3.2 Kutengeneza picha zenye ujumbe tofauti kwa jamii<br>3.3 Kubuni chapa mbalimbali za sanaa za ufundi<br>3.4 Kufinyanga maumbo mbalimbali |
| 4.0 Kufahamu stadi za ujasiriamali | 4.1 Kujenga utayari wa kujifunza<br>4.2 Kutafuta masoko ya bidhaa ndogondogo<br>4.3 Kutambua kanuni za usimamizi wa fedha |

**Jedwali Na. 7: Maudhui ya muhtasari Darasa la VII**

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wa wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| 1.0 Kuwa nadhifu | 1.1 Kujenga tabia ya usafi wa mwili | a) Kuaridhia utaratibu wa kutunza nywele zinazoota sehemu anuai za mwili kwa kuzingatia usahihi na usalama wa vifaa | Utaratibu wa kutunza nywele zinazoota sehemu anuia za mwili kwa kuzingatia usahihi na usalama wa vifaa umearidhiwa | Anataja sehemu anuai za mwili zinazoota nywele au vifaa sahihi vinavyotumika katika utunzaji wa nywele | Anatofautisha vifaa vinavyotumika katika utunzaji wa nywele zinazoota sehemu anuai za mwili | Anaelezea taratibu zinazotakiwa katika utunzaji wa nywele zinazoota sehemu anuai za mwili akizingatia usahihi na usalama wa vifaa | Anaaridhia taratibu zinazotakiwa katika utunzaji wa nywele zinazoota sehemu anuai za mwili akizingatia usahihi na usalama wa vifaa | 5 |
| | | b) Kufafanua uhifadhi wa vifaa vinavyotumika kujihifadhi wakati wa hedhi | Uhifadhi wa vifaa vinavyotumika kujihifadhi wakati wa hedhi umefafanuliwa | Anaorodhesha vifaa vinavyotumika kujihifadhi wakati wa hedhi | Anabainisha vifaa vinavyotumika kujihifadhi wakati wa hedhi | Anachanganua vifaa vinavyotumika kujihifadhi wakati wa hedhi | Anachanganua vifaa vinavyotumika kujihifadhi wakati wa hedhi na jinsi ya kuvihifadhi na kutoa mifano | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wa wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | | c) Kufafanua utunzaji wa mahali pa kulala na usafishaji wa matandiko husika | Utunzaji wa mahali pa kulala na usafishaji wa matandiko husika umefafanuliwa | Anataja mahali anuai pa kulala | Anaeleza mahali anuai pa kulala na usafishaji wa matandiko husika | Anaaridhia utunzaji wa mahali pa kulala akizingatia usafishaji wa matandiko | Anafafanua utunzaji wa mahali pa kulala na usafishaji wa matandiko na kutoa mifano | |
| | 1.2 Kutunza mavazi katika kudumisha usafi | a) Kuchanganua faida za kusafisha nguo na kupiga pasi na madhara ya kukiuka | Faida za kusafisha nguo na kupiga pasi na madhara ya kukiuka yamechanga-nuliwa | Anataja vifaa vinavyotumika kusafisha nguo au kupiga pasi | Anatofautisha vifaa vya kusafisha nguo na kupiga pasi | Anachanganua faida za kusafisha nguo na kupiga pasi na madhara ya kukiuka | Anachanganua faida za kusafisha nguo na kupiga pasi na madhara ya kukiuka na kutoa mifano | 5 |
| | | b) Kupambanua utaratibu wa kutunza nguo za ndani | Utaratibu wa utunzaji wa nguo za ndani umepambanuliwa na kutoa mifano | Anataja aina za nguo za ndani | Anaeleza utumiaji sahihi wa nguo za ndani | Anabaini utunzaji wa nguo za ndani akizingatia utumiaji sahihi, usafishaji na sehemu ya kuzihifadhi | Anapambanua utunzaji wa nguo za ndani akizingatia utumiaji sahihi, usafishaji, sehemu ya kuzihifadhi na kutoa mifano | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wa wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | | c) Kuchambua utaratibu wa utunzaji viatu | Utaratibu wa utunzaji wa viatu na hasara za kukiuka taratibu hizo umechambuliwa na kutoa mifano | Anaorodhesha vifaa vinavyotumika katika utunzaji wa viatu | Anaeleza utunzaji wa viatu pasipo kuhusisha hasara za kukiuka taratibu hizo | Anaelezea utaratibu wa utunzaji wa viatu na hasara za kukiuka taratibu | Anachambua utaratibu wa utunzaji wa viatu na hasara za kukiuka taratibu hizo na kutoa mifano | |
| | 1.3 Kutunza mazingira katika kudumisha makazi safi | a) Kuchanganua faida za kuwa na bustani katika makazi | Faida za kuwa na bustani katika makazi zimechanganuliwa | Anataja faida za kuwa na bustani katika makazi | Anaeleza faida za kuwa na bustani katika makazi | Anabaini faida za kuwa na bustani katika makazi | Anachanganua faida za kuwa na bustani katika makazi | 5 |
| | | b) Kuchambua faida zitokanazo na uhifadhi wa taka na madhara ya kukiuka na kutoa mifano | Faida zitokanazo na uhifadhi sahihi wa taka na madhara ya kukiuka yamechambuliwa na kutoa mifano | Anataja njia za uhifadhi sahihi wa taka au madhara ya kukiuka | Analinganisha faida zitokanazo na uhifadhi wa taka na madhara ya kukiuka | Anachambua faida zitokanazo na uhifadhi sahihi wa taka na madhara ya kukiuka | Anachambua faida zitokanazo na uhifadhi sahihi wa taka na madhara ya kukiuka na kutoa mifano | |
| | | c) Kuainisha njia za kudhibiti wadudu waharibifu wanaopatikana katika mazingira na kutoa mifano | Njia za udhibiti wa wadudu waharibifu wanaopatikana katika mazingira zimeainishwa na kutoa mifano | Anaorodhesha wadudu waharibifu wanaopatikana katika mazingira | Anabaini njia za kudhibiti wadudu waharibifu wanaopatikana katika mazingira | Anaainisha njia za kudhibiti wadudu waharibifu wanaopatikana katika mazingira | Anaainisha njia za kudhibiti wadudu waharibifu wanaopatikana katika mazingira na kutoa mifano | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wa wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| 2.0 Kumudu mapishi mbali-mbali | 2.1 Kutambua kanuni zinazohitajika katika mapishi mbalimbali | a) Kuchambua madhara yatokanayo na kukiuka kanuni za usafi katika mapishi | Madhara yatokanayo na kukiuka kanuni za usafi katika mapishi yamechambuliwa na kutoa mifano | Anataja kanuni za usafi katika mapishi pasipo kuhusisha madhara ya kukiuka | Anaeleza madhara yatokana na kukiuka kanuni za usafi katika mapishi | Anabainisha madhara yatokanayo na kukiuka kanuni za usafi katika mapishi | Anachambua madhara yatokanayo na kukiuka kanuni za usafi katika mapishi na kutoa mifano | 4 |
| | | b) Kufafanua madhara yatokanayo na kukiuka taratibu za kuzingatia wakati wa kula chakula | Madhara yatokanayo na kukiuka taratibu za kuzingatia wakati wa kula chakula yamefafanuliwa na kutolewa suluhisho | Anataja taratibu za kuzingatia wakati wa kula chakula | Anabainisha madhara yatokanayo na kukiuka taratibu za kuzingatia wakati wa kula chakula | Anafafanua madhara yatokanayo na kukiuka taratibu za kuzingatia wakati wa kula | Anafafanua madhara yatokanayo na kukiuka taratibu za kuzingatia wakati wa kula chakula na kutoa suluhisho | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wa wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | 2.2 Kutayarisha vyakula vya aina mbalimbali | a) Kuchambua madhara yatokanayo na kukiuka taratibu za kukaanga vyakula kwa mafuta mengi | Madhara yatokanayo na kukiuka taratibu za kukaanga vyakula kwa mafuta mengi zimechambuliwa na kutolewa suluhisho | Anabaini taratibu za kukaanga vyakula kwa mafuta mengi | Anaelezea madhara yatokanayo na kukiuka taratibu za kukaanga vyakula kwa mafuta mengi | Anachambua madhara yatokanayo na kukiuka taratibu za kukaanga vyakula kwa mafuta mengi | Anachambua madhara yatokanayo na kukiuka taratibu za kukaanga vyakula kwa mafuta mengi na kutoa suluhisho | 4 |
| | | b) Kuchanganua vyakula vya kufungasha na vifungashio vyake | Vyakula vya kufungasha na vifungashio vyake vimechanga-nuliwa | Anaorodhesha vyakula vya kufungasha | Anabainisha vyakula vya kufungasha | Anabainisha vyakula vya kufungasha na vifungashio sahihi akizingatia ubora na usalama wa vyakula | Anachanganua vyakula vya kufungasha na vifungashio vyake na kutoa mifano | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wa wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | 2.3 Kutengeneza vinywaji tofauti | a) Kufafanua faida za vinywaji baridi | Faida za vinywaji baridi zimefafanuliwa na kuhusisha mifano | Anataja aina za vinywaji baridi bila mifano | Anaorodhesha faida za vinywaji baridi na mifano yake | Anabainisha faida za vinywaji baridi | Anafafanua faida za vinywaji baridi akihusisha mifano | 5 |
| | | b) Kuandaa juisi ya matunda mchanganyiko | Juisi ya matunda mchanganyiko imeandaliwa kwa kuzingatia viambaupishi sahihi, ubora, vipimo sahihi, usafi na kuonesha ubunifu | Anaandaa juisi ya matunda mchanganyiko pasipo kuzingatia utaratibu unaotakiwa | Anaandaa juisi ya matunda mchanyanyiko akizingatia baadhi ya taratibu zinazotakiwa | Anaandaa juisi ya matunda mchanganyiko akizingatia viambaupishi sahihi, ubora, vipimo sahihi, usafi bila ya kuonesha ubunifu | Anaandaa juisi ya matunda mchanganyiko akizingatia viambaupishi sahihi, ubora, vipimo sahihi, usafi na kuonesha ubunifu | |
| | | c) Kuandaa kinywaji cha yai na pudini ya matunda | Pudini ya matunda na kinywaji cha yai kimeandaliwa kwa kuzingatia viambaupishi sahihi, ubora, usafi na kuongeza ubunifu | Anaandaa pudini ya matunda na kinywaji cha yai bila ya kufuata taratibu zinazotakiwa | Anaandaa pudini ya matunda na kinywaji cha yai akifuata baadhi ya taratibu zinazotakiwa | Anaandaa pudini ya matunda na kinywaji cha yai akifuata taratibu zote zinazotakiwa | Anaandaa pudini ya matunda na kinywaji cha yai akizingatia viambaupishi sahihi, ubora, usafi na kuongeza ubunifu | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wa wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| 3.0 Kusanifu kazi za Sanaa | 3.1 Kumudu misingi ya uimbaji na uigizaji | a) Kubaini mbinu za kuimba nyimbo katika kwaya ya sauti nne | Mbinu za kuimba nyimbo katika kwaya ya sauti nne zimebainishwa | Anataja mbinu za kuimba nyimbo katika kwaya ya sauti nne | Anaeleza mbinu za kuimba nyimbo katika kwaya ya sauti nne | Anabaini mbinu za kuimba nyimbo katika kwaya ya sauti nne | Anabaini mbinu za kuimba nyimbo katika kwaya ya sauti nne na kutoa mifano | 8 |
| | | b) Kuimba wimbo katika kwaya ya sauti nne | Wimbo umeimbwa katika kwaya ya sauti nne | Anaimba wimbo katika kwaya ya sauti moja | Anaimba wimbo katika kwaya ya sauti mbili | Anaimba wimbo katika kwaya ya sauti tatu | Anaimba wimbo katika kwaya ya sauti nne | |
| | | c) Kufafanua kanuni sita za kutunga igizo | Kanuni sita za kutunga igizo zimefafanuliwa | Anataja kanuni moja hadi tatu za kutunga igizo | Anaeleza kanuni sita za kutunga igizo | Anafafanua kanuni tano za kutunga igizo | Anafafanua kanuni sita za kutunga igizo | |
| | | d) Kutumia kanuni sita katika kutunga igizo fupi | Kanuni sita za kutunga igizo fupi zimetumika | Anatumia kanuni moja hadi mbili katika kutunga igizo fupi | Anatumia kanuni tatu katika kutunga igizo fupi | Anatumia kanuni nne hadi tano katika kutunga igizo fupi | Anatumia kanuni sita katika kutunga igizo fupi | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wa wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | | e) Kutumia kanuni sita za uigizaji kuigiza igizo | Kanuni za uigizaji zimetumiwa katika kuigiza igizo | Anatumia kanuni moja hadi mbili za uigizaji katika kuigiza igizo | Anatumia kanuni tatu za uigizaji katika kuigiza igizo | Anatumia kanuni nne hadi tano za uigizaji katika kuigiza igizo | Anatumia kanuni zote sita za uigizaji kuigiza igizo | |
| | 3.2 Kutengeneza picha zenye ujumbe tofauti kwa jamii | a) Kuchanganua maeneo sita yenye sifa za kuvutia upigaji wa picha za mnato za kibiashara na kutoa mifano | Maeneo sita yenye sifa za kuvutia upigaji picha za mnato za kibiashara yamechanga-nuliwa | Anataja maeneo sita ya kuvutia upigaji wa picha za mnato za kibiashara | Anabainisha maeneo sita yenye sifa ya kuvutia upigaji wa picha za mnato za kibiashara | Anaelezea maeneo sita ya kuvutia upigaji wa picha za mnato za kibiashara | Anachanganua maeneo sita ya kuvutia upigaji wa picha za mnato za kibiashara na kutoa mifano | 5 |
| | | b) Kutumia kanuni sita za upigaji picha, kupiga picha za mnato | Kanuni sita za upigaji picha za mnato zimetumika katika kupiga picha | Anapiga picha za mnato akizingatia kanuni moja hadi tatu za upigaji picha | Anapiga picha za mnato akizingatia kanuni nne za upigaji picha | Anapiga picha za mnato akizingatia kanuni tano za upigaji picha | Anapiga picha za mnato akizingatia kanuni zote sita za upigaji picha | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wa wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | | c) Kujadili maadili na taratibu za utunzaji wa picha za wateja kabla ya kuzigawa | Maadili na taratibu za utunzaji wa picha za wateja kabla ya kuzigawa yamejadiliwa | Anataja maadili na taratibu za utunzaji wa picha za wateja kabla ya kuzigawa | Anaeleza maadili na taratibu za utunzaji wa picha za wateja kabla ya kuzigawa | Anafafanua maadili na taratibu za utunzaji wa picha za wateja kabla ya kuzigawa | Anajadili maadili na taratibu za utunzaji wa picha za wateja kabla ya kuzigawa | |
| | 3.3 Kubuni chapa mbalimbali za Sanaa za ufundi | a) Kutumia vigezo kuchonga motifu | Motifu mbalimbali zimechongwa kwa kuzingatia vigezo na kuongeza ubunifu | Anachonga motifu akizingatia kigezo kimoja | Anachonga motifu akizingatia vigezo vichache | Anachonga motifu akizingatia vigezo vyote | Anachonga motifu mbalimbali akizingatia vigezo vyote na kuongeza ubunifu | 7 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wa wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | | b) Kutumia kanuni za uchapaji kuchapa motifu za maumbo mbalimbali | Kanuni za uchapaji zimetumiwa katika kuchapa motifu za maumbo ya jani, mnyama, kiganja cha mkono, unyayo na tunda | Anatumia kanuni moja hadi mbili za uchapaji kuchapa motifu za maumbo ya jani, mnyama, kiganja cha mkono, unyayo na tunda | Anatumia kanuni tatu za uchapaji kuchapa motifu za maumbo ya jani, mnyama, kiganja cha mkono, unyayo na tunda | Anatumia kanuni nne hadi tano za uchapaji kuchapa motifu za maumbo ya jani, mnyama, kiganja cha mkono, unyayo na tunda | Anatumia kanuni zote sita za uchapaji kuchapa motifu za maumbo ya jani, mnyama, kiganja cha mkono, unyayo na tunda | |
| | | c) Kutumia vigezo vinne vya upambaji kuandaa fremu ya utepe na kuiweka kwenye pambo la ruwaza | Vigezo vinne vya upambaji vimetumika katika kuandaa fremu ya utepe na kuiweka kwenye pambo la ruwaza | Anatumia kigezo kimoja katika kuandaa fremu ya utepe na kuiweka kwenye pambo la ruwaza | Anatumia vigezo viwili vya upambaji kuandaa fremu ya utepe na kuiweka kwenye pambo la ruwaza | Anatumia vigezo vitatu vya upambaji kuandaa fremu ya utepe na kuiweka kwenye pambo la ruwaza | Anatumia vigezo vinne vya upambaji kuandaa fremu ya utepe na kuiweka kwenye pambo la ruwaza | |
| | | d) Kuandaa fremu ya utepe | Fremu ya utepe inaandaliwa kwa vipimo sahihi na rangi za kuvutia | Anaandaa fremu ya utepe bila kuzingatia vipimo sahihi wala rangi za kuvutia | Anaandaa fremu ya utepe akizingatia vipimo sahihi au rangi za kuvutia | Anaandaa fremu ya utepe kwa kuzingatia rangi za kuvutia | Anaandaa fremu ya utepe kwa kuzingatia vipimo sahihi, na rangi za kuvutia na kuongeza ubunifu | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wa wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | 3.4 Kufinyanga maumbo mbalimbali | a) Kutumia vigezo vya ufinyanzi katika kufinyanga vifaa mbalimbali na kuonesha ubunifu | Vigezo vya ufinyanzi vimetumika katika kufinyanga chungu, bakuli, kikombe na chetezo | Anatumia kigezo kimoja katika kufinyanga chungu, bakuli, kikombe na chetezo | Anatumia vigezo viwili vya ufinyanzi kufinyanga chungu, bakuli, kikombe na chetezo | Anatumia vigezo vitatu vya ufinyanzi kufinyanga chungu, bakuli, kikombe na chetezo | Anatumia vigezo vinne vya ufinyanzi kufinyanga chungu, bakuli, kikombe na chetezo na kuonesha ubunifu | 5 |
| | | b) Kutumia vigezo vya urembaji kuremba vyombo vya nyumbani vilivyofinyangwa | Vigezo vya urembaji vimetumika katika kuremba vyombo vilivyofinyangwa | Anatumia kigezo kimoja katika kuremba vyombo vilivyofinyangwa | Anatumia vigezo vitatu vya urembaji kuremba vyombo vilivyofinyangwa. | Anatumia vigezo vinne hadi vitano vya urembaji kuremba vyombo vilivyofinyangwa | Anatumia vigezo vya urembaji kuremba vyombo vilivyofinyangwa kwa ubunifu | |
| | | c) Kutumia kanuni za uchomaji wa vyombo vilivyofinyangwa kuchoma vyombo katika tanuri la wazi | Uchomaji wa vyombo vilivyofinyangwa vimechomwa katika tanuri la wazi kwa kuzingatia kanuni za uchomaji | Anatumia kanuni moja hadi mbili katika kuchoma vyombo vilivyofinyangwa kwa udongo | Anatumia kanuni tatu za uchomaji wa vyombo vilivyofinyangwa kwa udongo | Anatumia kanuni nne hadi tano za uchomaji wa vyombo vilivyofinyangwa kwa udongo | Anatumia kanuni sita za uchomaji wa vyombo vilivyofinyangwa kwa udongo | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wa wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| 4.0 Kufahamu stadi za ujasiria-mali | 4.1 Kujenga utayari wa kujifunza | a) Kufafanua kanuni za ustawishaji bora wa mazao na ufugaji mifugo mbalimbali | Kanuni za ustawishaji bora wa mazao na ufugaji mifugo zimefafanuliwa | Anataja baadhi ya kanuni za ustawishaji bora wa mazao na ufugaji bora wa mifugo | Anaeleza baadhi ya kanuni za ustawishaji bora wa mazao na ufugaji bora wa mifugo | Anabaini kanuni za ustawishaji bora wa mazao na ufugaji bora wa mifugo | Anafafanua kanuni za ustawishaji bora wa mazao na ufugaji bora wa mifugo | 5 |
| | | b) Kubaini njia bora za kilimo na ufugaji wa mifugo mbalimbali | Njia bora za kilimo na ufugaji wa mifugo mbalimbali zimebainishwa | Anataja njia bora za kilimo na ufugaji wa mifugo mbalimbali | Anabainisha njia tatu za kilimo bora na njia tatu za ufugaji bora wa mifugo mbalimbali | Anabainisha njia nne bora za kilimo na ufugaji wa mifugo mbalimbali | Anabainisha njia zaidi ya nne bora za kilimo na ufugaji wa mifugo mbalimbali na kutoa mifano | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | **Utendaji chini ya wastani** | **Utendaji wa wastani** | **Utendaji mzuri** | **Utendaji mzuri sana** | |
| | | c) Kutayarisha bustani za aina mbalimbali za mboga. | Bustani za aina mbalimbali za mboga zimetayarishwa kwa kuzingatia utaratibu unaotakiwa na kuongeza ubunifu | Anatayarisha bustani za aina mbalimbali za mboga pasipo kuzingatia taratibu zinazotakiwa | Anatayarisha bustani za aina mbalimbali za mboga akizingatia baadhi ya taratibu zinazotakiwa | Anatayarisha bustani za aina mbalimbali za mboga akizingatia taratibu zote zinazotakiwa | Anatayarisha bustani za aina mbalimbali za mboga akizingatia taratibu zote zinazotakiwa na kuongeza ubunifu | |
| | 4.2 Kutafuta masoko ya bidhaa ndogondogo | a) Kufungasha bidhaa ndogondogo | Ufungashaji wa bidhaa ndogondogo umefanyika kwa kuzingatia vigezo vyote vya ufungashaji | Anafungasha bidhaa kwa kuzingatia vigezo viwili vya ufungashaji | Anafungasha bidhaa ndogondogo kwa kuzingatia vigezo vinne vya ufungashaji | Anafungasha bidhaa ndogondogo kwa kuzingatia vigezo vitano vya ufungashaji | Anafungasha bidhaa ndogondogo kwa kuzingatia vigezo sita vya ufungashaji wa bidhaa | 7 |
| | | b) Kubaini mbinu za kuvutia wateja na kutoa mifano | Mbinu za kuvutia wateja zimebainishwa na kutoa mifano | Anataja mbinu za kuvutia wateja. | Anaorodhesha mbinu za kuvutia wateja | Anaelezea mbinu za kuvutia wateja | Anabainisha mbinu za kuvutia wateja na kutoa mifano | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wa wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | | c) Kufafanua mbinu za kuzuia udanganyifu wa kibiashara unaofanywa na watu anaoshirikiana nao katika biashara | Mbinu za kuzuia udanganyifu wa kibiashara zimefafanuliwa na kutoa mifano | Anataja mbinu za kuzuia udanganyifu wa kibiashara | Anabainisha mbinu za kuzuia udanganyifu wa kibiashara | Anafafanua mbinu za kuzuia udanganyifu wa kibiashara | Anafafanua mbinu za kuzuia udanganyifu wa kibiashara na kutoa mifano | |
| | | d) Kujadili hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kumlinda mlaji dhidi ya bidhaa zilizoisha muda wa matumizi | Hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kumlinda mlaji dhidi ya bidhaa zilizoisha muda wa matumizi zimejadiliwa | Anataja hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kumlinda mlaji dhidi ya bidhaa zilizoisha muda wa matumizi | Anachanganua hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kumlinda mlaji dhidi ya bidhaa zilizoisha muda wa matumizi | Anafafanua hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kumlinda mlaji dhidi ya bidhaa zilizoisha muda wa matumizi | Anajadili hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kumlinda mlaji dhidi ya bidhaa zilizoisha muda wa matumizi na kutoa ufafanuzi | |
| | 4.3 Kutambua kanuni za usimamizi wa fedha | a) Kuchambua huduma za kifedha zitolewazo kwa njia ya benki | Huduma za kifedha zitolewazo na benki zimechambuliwa | Anataja aina za huduma za kifedha zinazotolewa na benki | Anaorodhesha huduma za kifedha zitolewazo na benki | Anaelezea huduma za kifedha zinazotolewa na benki | Anajadili huduma za kifedha zinazotolewa na benki | 5 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za mwanafunzi | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji wa Mwanafunzi | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji chini ya wastani | Utendaji wa wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | | b) Kuchanganua matumizi ya rejesta zinazotumika kutunza kumbukumbu za bidhaa na fedha | Matumizi ya rejesta zinazotumika kutunza kumbukumbu za bidhaa na fedha yamechanganuliwa | Anataja matumizi ya rejesta za kutunza kumbukumbu za bidhaa na fedha | Anaeleza matumizi ya rejesta za kutunza kumbukumbu za kifedha na bidhaa | Anabainisha matumizi ya rejesta zinazotumika kutunza kumbukumbu za bidhaa na fedha. | Anachambua matumizi ya rejesta zinazotumika kutunza kumbukumbu za bidhaa na fedha na kutoa ufafanuzi | |
| | | c) Kubainisha faida jamii inazopata kutokana na kulipa kodi | Faida jamii inayopata kutokana na kulipa kodi zimebainishwa | Anataja baadhi ya faida jamii inayopata kutokana na kulipa kodi | Anaorodhesha baadhi ya faida jamii inazopata kutokana na kulipa kodi | Anaelezea faida zote jamii inazopata kutokana na kulipa kodi | Anabainisha faida zote jamii inazopata kutokana na kulipa kodi | |